



## Umdhaniaye ...

- Joho:** kuna kitu nataka niwaambie, unajua muda sasa umepita tangu tumetoa yale matangazo, kwamba tunahitaji kuongeza msanii kwenye kikundi chetu.
- Wote:** Ndiyo tunajua, maana tupo wachache sana inabidi tuongeze wasanii wengine.
- Joho:** Hebu nikuulize ulipeleka lile tangazo kule Ngarasero?
- Kulu:** Ndiyo nilipeleka mpaka kwa mwenyekiti wa kijiji
- Joho:** Na wewe ulibandika lile tangazo?
- Mwaduga:** Ndiyo nilibandika
- Joho:** Sasa, nafikiri tufanye mazoezi maana kuna mtu anataka kujiunga na kikundi chetu
- Wote:** Tupige ngoma tuu watu watakuja tuu
- Mwaduga:** Sawa basi tupige taratibu tuu, watu watakuja
- Amina:** Piga bwana, tunataka kusikia ili watu waje
- Rukia:** Piga basi, (wakipiga ngoma na vigelegele)
- Chamaa:** Hebu subiri kwanza
- Mpita njia:** Habari zenu jamani?
- Wote:** Nzuri sana, karibu sana
- Mpita njia:** Samahani bwana, nimejaribu kupitapita nikasikia kuna kikundi cha ngoma
- Joho & Kulu:** Hapa umefika kabisa
- Wote:** Sasa mtu mwenyewe yuko wapi?
- Mpita njia:** Ni mimi jamani,
- Joho:** Sisi tulidhani unakuja kufadhili kikundi chetu?

- Mpita njia:** Hapana jamani, mimi ni msanii jamani.
- Joho:** Utaweza kweli wewe?
- Mpita njia:** Ndiyo nitaweza.
- Mwaduga:** Sisi tulidhani una ofisi na unafanya kazi na kompyuta—laptop.
- Mpita njia:** Samahani bwana mimi nimekuja rasmi kujiunga na nyie. Mimi ni msanii kama nyie kama mnatafuta watu, hata mimi ninaweza.
- Wakinadada:** Mzee utaweza kweli?
- Mpita njia:** Ndiyo naweza kabisa!
- Wakinadada:** Sawa basi vua viatu tuone!
- Mpita njia:** Mimi najua kucheza ngoma yejote.
- Joho:** Ataweza kweli, huyo au atatuonyesha laptop huyo?
- Wanakikundi:** Jamani tumpeni nafasi tuone, mtu mwenyewe hana ngoma wala nini? Ataweza kweli?
- Wakinadada:** Tumepata msanii mzuri kweli!
- Joho:** ataweza huyo kweli? Mimi hata siamini kabisa!
- Mpita njia:** (akicheza)
- Wanakikundi:** Hahaaha ... Umeweza kabisa! Hongera sana!
- Mpita njia:** Niliwaambia mimi ninaweza kabisa.
- Mwaduga:** Kweli kabisa unaweza sana, kuanzia leo wewe ni msanii wetu Kabisa
- Joho:** Karibu sana, kumbe umdhianiaye ndiye kumbe siye! Karibu sana, wewe ndiye bwana.
- Mpita njia:** Asante sana.
- Kulu:** Sasa itabidi tuendelee na mazoezi huenda wengine wakaja.
- Wanakikundi:** Sawa tuendelee tuu.